

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

Simu: +25526-230081
Nukushi: +25526-2321170
Barua pepe: km@habari.go.tz
Tovuti: www.habari.go.tz



S. L. P 25,
Mtaa wa Habari,
Mji wa Serikali Mtumba,
40481 Dodoma.

TAARIFA KWA UMMA

SALAMU ZA POLE

Dodoma - Februari 22, 2021

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) amepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Msanii Amri Bawji, ambaye amefariki dunia Februari 21, 2021.

“Hili ni pigo kwa wadau wa tasnia ya Sanaa nchini, tutamkumbuka Amri Bawji kwa kazi yake ya kuelimisha umma kupitia kazi zake za Sanaa,” amesema Mhe. Bashungwa.

Marehemu Amri Bawji atakumbukwa kwa kazi zake za uandishi wa kazi ya Sanaa ikiwemo Riwaya za Muafaka, Kubali Tuyamalize, Dunia Hadaa, Augua, Ua la Matumaini ambavyo vimekuwa ni darasa katika maisha ya kifamilia yanayosukumwa na upendo wa kweli katika familia na jamii nzima ya Watanzania.

Mhe. Bashungwa ametoa pole kwa Familia, Ndugu, Jamaa, Marafiki, Wasanii, Watunzi wa Vitabu pamoja na wadau wote wa tasnia ya Sanaa na anawaomba kwa Mwenyezi Mungu wote walioguswa na msiba huu wapate nguvu na moyo wa ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu.

Imetolewa na

Shamimu Nyaki

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo